

MTANGAMANO KAMA KIUNGO CHA MSHIKAMANO KATIKA DISKOSI ZA KIWINGI-LUGHA

Salim Sawe na Mosol Kandagor

Ikisiri

Mshikamano ni elementi muhimu ya kiisimu inayochangia ufasili wa maana katika diskosi. Makala hii, hivyo basi, inafafanua jinsi mtangamano unavyohusika kama kiungo cha mshikamano katika diskosi za kiwingi-lugha. Nadharia Amilifu Zalishi ilitumiwa katika uchunguzi huu (Sawe, 2015). Nadharia hiyo inasisitiza kwamba uunganishaji, uradidi na mtangamano ni mikakati inayojenga mshikamano katika matini au diskosi huku ikipinga dai kwamba udondoshaji ni kijenzi cha mshikamano. Data ilikusanywa kutoka sampuli ya makanisa mawili na vyo vikiu viwili nchini Kenya. Diskosi za kiwingi-lugha za wanafunzi waliozungumza Kiswahili, Kikipsigis na Kiingereza zilichunguzwa. Utafiti huu uligundua kwamba wanawingi-lugha hutumia mtangamano kama mojawapo ya mikakati ya kuendeleza mshikamano katika mazungumzo yao yenye ubadilishaji msimbo.

Utangulizi

Makala hii ilitokana na uchunguzi wa wanawingi-lugha waliokuwa wakibadilisha msimbo baina ya Kiswahili, Kiingereza na Kikipsigis nchini Kenya. Makala hii imetumia dhana ‘diskosi za wingi-lugha kurejelea diskosi zenye Ubadilishaji msimbo (U.M.) zilizochunguzwa katika utafiti huo. Mchango wa mtangamano kwa ujenzi wa mshikamano haujaendelezwa katika tafiti nyingi. Kwa mfano, watafiti kama vile Hasan (1984), Halliday (1985), Hoey (1991), Martin (1992), Omogo (1996) na Makoti (2013) hawakushirikisha mkakati wenyewe katika ubainishaji wa viungo vya mshikamano katika matini.

Watafiti kadhaa wamehitimisha kwamba mazungumzo yanayoshirikisha U.M. hayana muumano. Hutukia kiholelaholela na, wakati mwingine, huwa hayajakamilika (Weinreich, 1953; Gardner-Chloros & Edwards, 2004 na Murray na wenzake, 2006). Mahitimisho yao yanadokeza kwamba mazungumzo ya wanawingi-lugha wanaobadilisha msimbo hayana mshikamano na muwala na; kwa fahiwa hiyo, hayadhahirishi mtangamano. Clyne (1987) anapinga dai kwamba mazungumzo yanayogeukageuka kama yale yenye U.M. yanaweza kufafanuliwa kisarufi kwa jinsi sawa na vipashio vya kiumoja-lugha. U.M. umeweza kurejelewa kama ishara ya uchafuzi wa lugha, uchachawizaji na utowekaji wa lugha. Hali hii ilichochea uchunguzi huu wa mtangamano kama mkakati wa kuibua mshikamano katika diskosi za kiwingi-lugha.

Msingi wa Nadharia

Uchunguzi huu wa mtangamano kama mkakati wa kuibua mshikamano katika diskosi za kiwingi-lugha uliongozwa na Nadharia Amilifu-zalishi [NAZ] (Sawe, 2015). Nadharia hii inazingatia mikakati mingi kuliko ile inayojitokeza katika nadharia nyingine za mshikamano kama ile iliyopendekeza na Halliday na Hasan (1976) na Hasan (1984). Kwa mujibu wa mwongozo huo wa kinadharia [NAZ], mikakati ya kuunganisha diskosi za lugha inaweza kuainishwa chini ya aina mbili kuu ambazo ni: (a) uradidi na (b) mtangamano. Sehemu mbalimbali za diskosi moja, kwa mujibu wa nadharia hii, huweza kushikamanishwa kwa kufanya uradidi kupitia: [i] ubadalia; [ii] uradidi sahili na changamano; [iii] haipanimu au hiponimu, [iv] usawe, [v] uwakilishaji; [vi] unyume (unaochukuliwa hasa kama urudiaji changamano) na [vii] meronimu.

Muwala, kwa mujibu wa NAZ, haujengwi kwa kutumia mshikamano pekee, ila unadhihirishwa kupitia (i) mpangilio thabiti wa vijenzi, (ii) muumano baina ya vitendo na vihusika vyao, na (iii) ufafanuzi wa ziada. Makala hii imechunguza namna nguzo hii (mtangamano) inavyochangia mshikamano wa kileksika katika diskosi za kiwingi-lugha. Diskosi za wanawingi-lugha zilichanganuliwa ili kubainisha namna mkakati huu unavyotumiwa katika mazungumzo yenye U.M.

Mbinu za Utafiti

Data ilikusanywa kutoka sampuli ya makanisa mawili na vyo viko viwili nchini Kenya. Mazungumzo ya kiwingi-lugha yalichunguzwa katika sampuli ya bewa moja moja kwa kila chuo kilichoteuliwa katika utafiti huu. Diskosi zenye U.M. zilichunguzwa vilevile katika makanisa mawili yaliyoteuliwa. Diskosi za kiwingi-lugha za wanafunzi waliozungumza Kiswahili, Kikipsigis na Kiingereza zilichunguzwa. Matumizi ya misimbo kama M1B1 au M1K1 katika makala hii yanarejelea namba ya siri ya mtafitiwa (M^x) katika eneo la utafiti—Kanisa (K^x) au Bewa (B^x). Diskosi zenye U.M. zilizohusisha Kiswahili, Kiingereza na Kikipsigis pekee zililengwa katika uchunguzi huu.

Dhana ya Mtangamano

Istilahi hii ilitumiwa katika makala hii kurejelea uteuzi wa kimantiki wa vijenzi vinavyounganishwa ili kuunda diskosi. Dhana hii inahusu hali ambapo maneno yanaweza kutangamana kimuundo pasi na mgongano wa kimantiki. Mtangamano ulitumiwa na watafitiwa ili kuibua mshikamano wa kileksika kwa kuviunganisha vipashio vinavyokubali ujirani au ushirikiano katika ujenzi wa muundo.

Wachanganuzi wengi kama vile McCarthy (1988), Hoey (1991) na Hasan (1984) walipuuza mtangamano katika uchanganuzi wao wa mshikamano wa kileksika. Utafiti huu uligundua kwamba mtangamano ni mkakati muhimu wa kujenga diskosi

za kiwingi-lugha zenye mshikamano kama inavyoonyeshwa katika sehemu ifuatayo inayobainisha aina zake.

Aina za Mtangamano

Sehemu ifuatayo inachanganua namna nguzo hii ilivyochangia mshikamano katika diskosi za watafitiwa kwa kuzingatia aina za mtangamano zilizobainika. Aina zinazofafanuliwa ni: mtangamano wa kikronolojia, mtangamano wa muktadha, mtangamano wa matukio, na mtangamano wa vinyume.

Mtangamano wa Kikronolojia

Mtangamano wa kikronolojia unahusu miambatano inayojitokeza katika diskosi kwa mujibu wa wakati au vipindi. Aina hii ya mtangamano inahusu seti za virejelewa vya kileksika kama vile nambari, miezi, na siku za wiki. Seti hizi zilishuhudiwa katika diskosi za watafitiwa ingawa zilitumiwa kwa asilimia ndogo kuliko viunganishi na viwakilishi. Usemi (1) wa M29B2 ufuatao unaonyesha namna mtangamano wa kikronolojia unavyochangia mshikamano. Mfano huu ulinukuliwa kutoka mazungumzo ya watafitiwa katika bewa la pili lililochunguzwa katika utafiti huu.

1. M29B2: *Zile records* nilikutumia juzi *were forwarded just yesterday. We have no otherwise but to reorganize ourselves.* Mkutano wenyewe tungefanya leo tutaipostpone mpaka kesho, na yale tungefanya kesho tuyaahirishe tena mpaka kesho kutwa. *All these means that those returns* **che konyolu kiyokten koron koyoche kiyokten koyoin.**

‘Zile rekodi nilizokutumia juzi zilipitishwa hiyo jana tu. Hatuna budi ila tujipange tena. Mkutano wenyewe ambao tungeufanya leo tutauahirisha mpaka kesho, yale ambayo tungeyafanya kesho tuyaahirishe tena mpaka kesho kutwa. Haya yote yanamaanisha kuwa tutawasilisha kesho kutwa zile taarifa tulizohitajika kuziwasilisha kesho.’

Mtangamano wa kikronolojia uliotokana na seti za vielezi vya wakati katika diskosi (1) umechangia mshikamano wa kileksika. Maneno yaliyosababisha mtangamano wa aina hii katika mfano (1) yaliendeleza mwandamano ingawa yaliteuliwa na mzungumzaji kutoka Kiswahili, Kiingereza na Kikipsigis. Maneno hayo ni pamoja na ‘juzi’ lililotangamana na ‘*yesterday*’ (jana) katika sentensi ya kwanza; ‘leo’ lililotangamana na ‘kesho’ katika sentensi ya pili na ‘**koron**’ (kesho) lililotangamana na ‘**koyoin**’ (kesho kutwa). Mtangamano huu ulijenga mshikamano ndani ya sentensi moja moja na baina ya sentensi zilizoshirikiana ili kujenga diskosi (1). Hatimaye, mtangamano huchangia kuibuliwa kwa muwala kwa sababu ufasiri wa sentensi moja hufanywa kwa mujibu wa ufasiri wa sentensi nyingine. Mfano (2) unaonyesha mtangamano wa kikronolojia uliotokana na majina ya siku za wiki.

2. M24B1: Eh! Umekuwa wapi wewe all this time?
'Eh! Umekuwa wapi wewe wakati huu wote?'

M25B1: *We've had a busy week I tell you. Mmh! Monday mpaka Wednesday tulikuwa na audit ya ISO. Thursday tulikuwa tukiedit curriculum until evening. Members' day mpaka Jumamosi tumeshinda hapa na mambo ya results. Sometimes, it is hard to find time to enjoy even what you earn.*

'Tumekuwa na wiki yenye shughuli nyingi ninakuambia. Mmh! Jumatatu mpaka Jumatano tulikuwa na ukaguzi wa ISO. Alhamisi tulikuwa tukihariri mtalaa mpaka jioni. Ijumaa mpaka Jumamosi tumeshinda hapa na mambo ya matokeo. Wakati mwingine, ni vigumu kupata hata wakati wa kufurahia ujira wako.'

M24B1: Yaani kila siku mpaka weekend, hata Jumapili hamna. Kanisa uliacha kwenda kwani? Wewe utaolewa na kazi!


'Yaani kila siku mpaka wikendi, hata Jumapili hamna. Kanisani uliacha kwenda kwani? Wewe utaolewa na kazi!'

M25B1:Lakini unajua kazi ni mume mbaya inakutaliki wakati wowote ikichelewa kukutaliki inangojea ukiwa umepoteza nguvu at 60; hapo watasema ustaafu na hiyo itakuwa Sunday ya kweli.

'Lakini unajua kazi ni mume mbaya inakutaliki wakati wowote. Ikichelewa kukutaliki, inangojea ukiwa umepoteza nguvu unapofikia miaka sitini; hapo watasema ustaafu na hiyo itakuwa Jumapili ya kweli.'

Mtangamano wa kikronolojia katika mfano (2) uliendeleza mshikamano wa kileksika kupitia matumizi ya vipashio vya kileksika vinavyohusu wiki kama week, Monday, Wednesday, Thursday, Members' day (Ijumaa), Jumamosi na Sunday (Jumapili). Maneno haya yaliyotumiwa na watafitiwa M24B1 na M25B1 katika zamu zao mbalimbali yanatangamana kwa sababu yanataja wiki na siku zake. Mtangamano wa kikronolojia katika diskosi hiyo umetumiwa pamoja na mikakati mingine kama vile uwakilishaji, uunganishaji na uradidi ili kuibua mshikamano. Kielelezo (1) kinaonesha namna mtangamano ulivyochangia kuibua mshikamano katika diskosi za kiwingi-lugha mintarafu ya diskosi (2) hapo juu.

Kielelezo Na. 1: Mtangamano wa Kikronolojia



Maumbo yanayounganisha leksimu katika kielelezo 1 yanaashiria kule kuwapo kwa mtangamano baina yao. Kielelezo chenyewe (1) kinadhihirisha namna leksimu mbalimbali zinazohusiana kifahiwa zinavyoweza kutumiwa na wanawingi-lugha ili kujenga mtangamano wa kikronolojia. Ingawa leksimu zingine ni za Kiswahili huku zingine zikiwa za Kiingereza, kuhusiana kwao kifahiwa kumechangia kuendeleza mtangamano na, kwa misingi hiyo, kuendeleza mshikamano wa kileksika.

Mtangamano wa Muktadha

Mtangamano wa aina hii ulidhihirika vilevile kama kijenzi cha mshikamano wa diskosi za watafitiwa kupitia matumizi ya miambatano ya maneno yanayohusiana kimazingira kama vile dereva na kusafiri, hospitali na wagonjwa, mwanafunzi na mwalimu na, hatimaye, taa na mwangaza. Jozi hizi za maneno zinazolingia kwenye mtangamano, zina mahusiano ya kisemantiki. Miambatano ya maneno inayotangamana imepigwa mistari katika mfano (3) ili kubainisha namna inavyotumiwa katika diskosi za kiwingi-lugha kuendeleza mshikamano.

3. M26B1: **Kalian oh Leah, le kaibur en yu for long ako kokobek time. Kolelen tos karimande by now?**

‘Ilikuwa je Leah, mbona umekaa kwa muda mrefu ilihali wakati umeisha. Nilidhani ungekuwa umetoka kufikia sasa?’

M27B1: Tunahitajika kusafirisha vyombo hivi lakini *driver* wa ambulance hajafika. Alimchukua *that last patient we were attending to* kwa hospitali but I understand that nurses wengi hawapo. Wao wamengojea kuhudumiwa na daktari mmoja anayemjua. **Kamatoki dischargeeni** lakini **ingoadmiten kityok echek asi kecheng’ a clinic ne nekit asikonyaiwech.**

‘Tunahitajika kusafirisha vyombo hivi, lakini dereva wa ambulensi hajafika. Alimchukua yule mgonjwa wa mwisho tuliyekuwa tukimshughulikia hospitalini, lakini nimearifiwa kwamba wahudumu hawapo. Wao wamengojea kuhudumiwa na daktari mmoja anayemjua. Hatungemwacha, lakini wacha alazwe tu ili tuitafute kliniki ya karibu imhudumie.


M26B1: **Kobokoyoe ng’o diagnosis** ili tujue anaumwa na nini? Si unajua ni kama tulimfanyia *first aid* na kumpatia pain killers tu. Hizo ni dawa za kudanganya mwili, hazitibu ugonjwa?

‘Nani atampima ili tujue anaumwa na nini? Si unajua ni kama tulimfanyia huduma ya kwanza na kumpatia dawa za maumivu tu. Hizo ni dawa za kudanganya mwili, hazitibu ugonjwa?’

Maneno mengi yaliyotumiwa, hasa katika usemi wa M27B1 katika mfano (3), yana mtangamano. Hii ni kwa sababu yanahusiana na mazingira ya hospitali. Kwa mfano, ambulensi (*ambulance*), ni gari la kutumiwa hospitalini, mgonjwa (*patient*) ni mtu anayetafuta matibabu hospitalini, wahudumu (*nurses*) na neno lenyewe ‘hospitali’ yameingia katika mtangamano unaoendeleza mshikamano katika matamko ya M27B1 yanayochangia diskosi (3) kama inavyosawiriwa katika kielelezo (2). Maneno haya yote yana mahusiano ya kisemantiki. Kwa hivyo, kutumiwa kwao kunachangia katika diskosi.

Maneno mengine yaliyotumiwa katika diskosi (3) yanadhihirisha mtangamano kwa sababu yanamhusu mgonjwa. Maneno hayo ni pamoja na *first aid*, kuhudumiwa, kuumwa, daktari, *diagnosis*, **keadmitten** (kumsajili mgonjwa), **dischargeen** (kumruhusu mgonjwa atoke hospitalini), *clinic* (kliniki), dawa, tibu, na *pain killers*. Kutumiwa kwa maneno hayo katika zamu mbalimbali za Diskosi (3) kunachangia mshikamano kupitia mtangamano unaojitokeza baina yao. Mtangamano unaojitokeza kwa jinsi hii katika diskosi nzima, vilevile, unaoendelea muwala wa diskosi zenye U.M. Kielelezo (2) kinaonesha namna mtangamano unavyochangia mshikamano katika diskosi ya kiwingi-lugha.

Kielelezo na. 2: Mtangamano wa Mukadha



Kielelezo na. 2 kinashiria jinsi maneno yaliyotumiwa na watafitiwa M26B1 na M27B1 yanavyochangia mshikamano kupitia mtangamano unaojitokeza baina yao. Laini zinazounganisha maneno hayo katika kielelezo zinaashiria kuwapo kwa mtangamano baina yao.

Mtangamano wa Matukio

Ufafanuzi wa mtangamano wa matukio uliotolewa na Halliday na Hasan (1976) una upungufu kwa sababu haubainishi ni faridi zipi zinazohusiana na zipi hazihusiani. Mtangamano wa matukio ni namna ambavyo watu, matendo, mahali, vitu au sifa huhusiana na matukio au vitendo vingine (Tanskanen, 2006). Kwa mfano, nomino zifuatazo zinaweza kusimbuliwa katika diskosi kiutangamano na vitenzi vianavyoambatana navyo: nguo zinaweza kuvaliwa, mikate ikaliwa na magari yakaendeshwa. Mifano (4) na (5) ifuatayo ya diskosi iliwahusisha watafitiwa M7K1 na M1K2, mtawalia; na inaonyesha namna ambavyo watafitiwa walikuwa

wakitumia mtangamano wa matukio katika kushikamanisha vipande vya mazungumzo yao:

4. M7K1: *I think it was good for us to be colonized first, our precolonial freedom was not true freedom. Africa was full of darkness; hebu fikiria hata wewe, mwangaza tuliopata kupitia education. Africa or any other part of the world ingekuwaje by now with completely no formal education.*

‘Ninafikiri kwamba ilifaa tutawaliwe na wakoloni kwanza. Uhuru tuliokuwa nao kabla ya kuja kwa wakoloni haukuwa uhuru wa kweli. Afrika ilikuwa imegubikwa na giza; hebu fikiria hata wewe mwangaza tuliopata kupitia elimu. Afrika au sehemu nyingine yoyote ya ulimwengu ingekuwaje kwa sasa bila elimu rasmi kabisa.’

5. M1K2: *She was seriously sick of cancer, had no appetite and every time she swallowed anything. Alikuwa anatapika. We were running out of options. Doctors had given up on her. Soon a nurse came and prayed over her in the name of Jesus, akaponywa tu hivyo.*

‘Yeye alikuwa mahututi akiugua ugonjwa wa saratani. Hakuwa na hamu ya chakula na wakati wote angemeza \chochote angetapika. Tulikuwa tumeshindwa la kufanya. madaktari walikuwa wamekata tamaa juu yake. Punde muuguzi mmoja alikuja na akamwomba kwa jina la Yesu, akaponywa tu hivyo.’

Diskosi (4) na (5) zinaonesha namna mshikamano wa kileksika unavyoibuliwa kwa matumizi ya mtangamano wa vitendo. Mtangamano katika Diskosi (4) umeibuliwa kwa matumizi ya mofimu nne zinazohusiana na matukio maalum. Kwa mfano, neno ‘colonized’ (tawaliwa) linatangana na tukio la kupata uhuru (*freedom*) katika sentensi ya kwanza. Pili, hali ya ‘kufunikwa na giza’ (*darkness*) inatangamana na tukio la kupatikana kwa ‘mwangaza’ katika sentensi ya pili.

Mtangamano wa matukio katika Diskosi (5) unajitokeza kwa njia kadhaa. Kwanza, hali ya kuwa ‘mgonjwa’ (*sick*) inatangamana na kitendo cha ‘kutapika’ ambacho, aghalabu, huwa ishara ya ugonjwa. Pili, tukio au kitendo cha kumeza (*swallowed*) kinatangamana na kitendo kinachokikanusha ‘kutapika’. Isitoshe, hali ya kuwa mgonjwa (*sick*) inatangamana na kitendo cha ‘kuponywa’. Matumizi ya maneno haya yanayotangamana kisemantiki na mengine huendeleza umoja katika diskosi za kiwingi-lugha.

Mtangamano wa Vinyume

Mtangamano wa vinyume unarejelea mwambatano wa kimfosintaksia, ambapo maneno yanayotumiwa kuunda diskosi hutokea katika ujozi. Mtangamano wa aina

hii ulitumiwa na watafitiwa kwa namna ambavyo maneno fulani yaliyoambatana katika mazungumzo yao yalikuwa yanahusiana kimazingira. Maneno yanayotangamana kwa njia hii, katika diskosi, huchangia muumano baina ya viambajengo vya diskosi zenye tajawuri za lugha kwa sababu ya kuwepo kwa uhusiano wa kukamilishana baina ya maneno yanayotumiwa.

Mtangamano wa vinyume uliodhihirika katika utafiti huu, kwa kiwango kikubwa, ulihusu mahusiano ya kiantonimia kama vile mwangaza na giza, mchana na usiku, nje na ndani, urefu na ufupi au chini na juu. Sehemu zilizopigwa mistari katika mfano (6) ufuatao, zinaashiria mtangamano wa unyume:

6. M6K5: **Kitinye** *authorithy as parents from God to bless our children.* **King’at**
Jehovah kole nyolu kohonouren lagook the parents si konyor
koyomiset.

‘Tuna mamlaka kutoka kwa Mungu kama wazazi ya kuwabariki watoto wetu. Mungu aliamuru kwamba watoto wanapaswa kuwaheshimu wazazi ili wapate ahadi.’

Mshikamano baina ya viambajengo vinavyojenga diskosi (6) umejengwa kwa kutumia maneno mawili yanayohusiana kifahiwa kama vinyume. Maneno hayo yanayotangamana ni ‘*parents*’ (wazazi) na ‘**lagook**’/ ‘*children*’ (watoto).

Mikufu ya kileksika ilitumiwa na watafitiwa ili kuibua mtangamano wa vinyume ambao, pamoja na viungo vingine, ulichangia uzalishaji wa diskosi za kiwingi-lugha zenye mshikamano. Mfano (7) ambao ni sehemu ya diskosi iliyozalishwa na watafitiwa katika bewa la kwanza, unaonesha mtangamano wa vinyume. Hata hivyo, muwala umechangiwa na aina nyingine za mtangamano katika mfano wenyewe. Mathalani:


7. M28B1: *Last night* tulisafiri na yule mwalimu wa *Geography*. Alikuwa na *lecture* mpaka *six thirty and darkness was approaching as we left the campus*. Alianza kulalamika juu ya yule *mechanic*. Alipojaribu kuwakisha taa za gari yake: za mbele zilikuwa *dim* na *brake lights* hazikuwa zinafanya kazi. Tulichokorachokora *head lamps* na *battery* but it was of no help at all. It was getting late and traffic jam was building up. Cars were hooting from behind. Aliendesha gari at a speed of almost 10 kilometres per hour. Nilimhurumia tu kwa vile hata mimi singependa kujidrive usiku in a situation like that, hata kama I like overspeeding during the day; I fear reckless night drivers. At last mafuta yaliisha na hakukuwa na petrol station karibu. We walked for some kilometres; uzuri there were many pedestrians

walking back home. Some were walking very fast but others seemed to have no hurry at all, walikuwa wanatembea polepole tu.

‘Jana usiku tulisafiri na yule mwalimu wa Jiografia. Alikuwa na mhadhara mpaka saa kumi na mbili unusu na giza lilikuwa linaingia tulipokuwa tukiondoka kutoka chuoni. Alianza kulalamika juu ya yule fundi. Alipojaribu kuwasha taa za gari yake: za mbele, zilikuwa zikififia na taa za breki hazikuwa zinafanya kazi. Tulichokorachokora taa za mbele na betri bure bilashi. Tulikuwa tumechelewa na msongamano wa magari ulikuwa unaendelea kuwa mkubwa. Magari yalikuwa yanapiga honi kutoka nyuma. Aliendesha gari kwa mwendo wa karibu kilomita 10 kwa saa moja. Nilimhurumia tu kwa vile hata mimi nisingependa kujiendesha usiku katika hali kama hiyo yake hata kama huwa ninapenda kuendesha kwa kasi zaidi mchana. Ninawaogopa madereva wanaoendesha bila hadhari usiku. Mwishowe mafuta yaliisha na hakukuwa na stesheni ya petroli karibu. Tulitembea kwa kilomita kadhaa; uzuri kulikuwa na watu waliokuwa wakitembea kwa miguu wakirudi nyumbani. Wengine walikuwa wakitembea kwa kasi sana, lakini wengine hawakuwa na haraka kabisa. Walikuwa wanatembea polepole tu.’

Kielelezo na. 3 kinawakilisha diskosi (7) iliyonukuliwa hapo juu kwa kuonyesha jinsi mtangamano unavyosababisha mshikamano katika diskosi za wanawingilugha. Mistari inayounganisha neno moja kwa lingine katika kielelezo inaonyesha namna muungano wa kisemantiki unavyojengwa katika akili za wasikilizaji ili waweze kuzifasiri sehemu zote za usemi kama vijenzi vyenye unamu vinavyounda diskosi moja.

Kielelezo 3: Mtangamano wa Vinyume



Kielelezo na. 3 kinachodhihirisha mtangamano wa vinyume, kinaonyesha kuwapo kwa muungano katika usemi huu unaohusu kutumiwa kwa jozi za maneno ambayo fahiwa zao zinapingana kwa pamoja kama vijenzi vya diskosi. Maneno yanayoingia katika mtangamano wa unyume katika kielelezo hiki ni *walk - drive, no hurry/polepole - fast; pedestrians - drivers; 'darkness' na 'taa'/'lights'*, kujidrive na kutembea. Maumbo haya ambayo yana mahusiano ya kifahiwa, yanachangia mshikamano.

Imebainika, katika utafiti tulioufanya, kwamba mikakati mbalimbali hutumiwa kujenga diskosi za wanawingi-lugha zenye mshikamano. Hata hivyo, kama inavyojitokeza katika mfano (8) ufuatao, mshikamano pekee hautoshelezi ili diskosi ijitosheleze kuwa diskosi. Yaani, udiskosi wa diskosi hautegemei mikakati ya mshikamano kama uunganishaji, uwakilishaji na uradidi pekee. Kinyume na alivyodai Halliday na Hasan (1976) kwamba umatini wa matini hutegemea mshikamano, mfano (8) unadhihirisha mshikamano unaoibuliwa kupitia uradidi, lakini haufasiriki (hauna muwala) kwa vile haujatimiza masharti yote ya udiskosi.

8. **My first born ana thirteen years. Thirteen is an odd number. Kuwa namba thirteen is everybody's favourite.*

Mtoto wangu wa kwanza ana miaka kumi na tatu. Kumi na tatu ni namba witi. Kuwa na namba kumi na tatu ni chagua la kila mtu.

Mfano (8) unadhihirisha mshikamano wa kileksika unaotokana na mtangamano baina ya 'kuwa kifungua mimba' (*first born*) na 'umri wa miaka kumi na mitatu' (*thirteen years*). Uradidi umechangia mshikamano huo kupitia kurudiwa kwa neno '*thirteen*' na kurudiwa kwa neno '*number*' kama 'namba'.

Hitimisho

Makala hii inahitimisha kuwa mtangamano ni mkakati wa kimshikamano unaoweza kutumiwa na wanawingi-lugha katika uwasilishaji wa maana. Mkakati huo una uamilifu wa kuunganisha seti za taarifa zinazopitishwa kwenye viambajengo mbalimbali. Mtangamano hufanywa kiuteuzi kwa namna ambavyo kipashio kinachotumiwa katika sehemu moja ya diskosi kinaambatana na kipashio kingine kinachohusiana nacho. Kutangamana kunakojitokeza baina yao huendeleza mshikamano.

Mtangamano huhakikisha kwamba kuna uhusiano wa kimaudhui baina ya viambajengo vya mazungumzo vinavyoshiriki katika diskosi nzima. Uteuzi na matumizi ya viambajengo vinavyotangamana ni mfanyiko wa kisaikolojia na wa kintindo unaofanyika kwa hiari katika akili za wazungumzaji. Matumizi ya mtangamano katika mazungumzo hujenga muktadha ufao kwa uwasilishaji wa ujumbe katika mchakato mzima wa mawasiliano kwa vile yanachangia ufasiri wa diskosi.

Marejeleo

- Clyne, M. (1987). “Constraints on Code-Switching: How Universal are They?” *Linguistics*, 25: 739 - 64.
- Gardner-Chloros, P. na M. Edwards (2004) “Assumptions behind the Grammatical Aspects to Code Switching: When the Blue Print is a Red Herring”. *Transactions of the Philological Society*, 102(1) 103 - 129.
- Halliday, M. (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.
- Halliday, M. na R. Hasan (1976). *Cohesion in English*. London: Longman.
- Hasan, R. (1984). “Coherence and Cohesive Harmony.” katika J. Flood (mh.), *Understanding Reading Comprehension: Cognition, Language and the Structure of Prose*. (181- 219). New York: Newark International Reading Association.
- Hoey, M. (1991). *Patterns of Lexis in Texts*. Oxford: Oxford University Press.
- Makoti, V. (2013). *Mshikamano wa Kisarufi katika Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Moi: Tasnifu ya Uzamivu (hajachapishwa).
- Martin, J. (1992). *English Text: System and Structure*. Amsterdam: Benjamins.
- McCarthy, M. (1988). “Some Vocabulary Patterns in Conversation.” katika R. Carter & M. McCarthy (Wah.), *Vocabulary and Language Teaching* (181-200). London: Longman Publishers.
- Murray, G. na Taboada, M. na S. Renals (2006). Prosodic Correlates of Rhetorical Relations. Proceedings of the Analyzing Conversations in Text and Speech (ACTS) Workshop at HLT-NAACL. New York City, New York, June 2006. 2006 Association for Computational Linguistics. 3(1 - 7). http://www.Murray_etal_NAACL_2006_Workshop.pdf [22.02.2013]
- Omogo, B. (1996). *Dhima ya Ushikamano katika Utendaji kwenye Insha za Kiswahili za Wanafunzi wa Kidato cha Nne Wilayani Kisii, Kenya*. Chuo Kikuu cha Moi: Tasnifu ya Uzamili ambayo hajachapishwa.
- Sawe, S. (2015). *Mshikamano na Muwala katika Diskosi za Wanawingi-lugha: Hali katika Vyuo Vikuu Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo hajachapishwa: Chuo Kikuu cha Laikipia.
- Tanskanen, S. (2006). *Collaborating towards Discourse: Lexical Cohesion in English*. Amsterdam: Benjamins Publishers.
- Weinreich, U. (1953). *Languages in Contact: Findings and Problems*. The Hague: Mouton.